

SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 51 **JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC)** MEI 2025

RAIS SAMIA SULUHU HASSAN ATOA NEEMA KWA WATUMISHI WA UMMA, ATANGAZA ONGEZEKO LA KIMA CHA CHINI CHA MSHAHARA



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Dkt. Samia Suluhu Hassan akipungia mkono maandamano ya watumishi mbalimbali (hawapo pichani) wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wafanyanyakazi Duniani iliyoadhimishwa kitaifa mkoani Singida tarehe 1 Julai, 2025.

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz

ASANTE SANA RAIS SAMIA KWA KUBOresha MASLAHI YA WATUMISHI WA UMMA

Tarehe 1 Mei, 2025 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa mgeni rasmi katika kilele cha maadhimisho ya siku ya Wafanyakazi Duniani alitangaza ongezeko la kima cha chini cha mshahara kwa watumishi wa umma kwa asilimia 35.1

Nyongeza hiyo itakayoanza mwezi Julai mwaka 2025 itaongeza kima cha chini cha mshahara kutoka 370,000 hadi Tsh. 500,000.

Bila shaka taarifa hizi zimepokelewa kwa shwangwe kubwa na watumishi wa umma kwa kuwa maisha yao yanakwenda kuwa bora zaidi.

Kabla ya kutangaza ongezeko hilo, Rais Samia alianza kuwasifia watumishi kwa uvumilivu wao namna wanavyojitoa kufanya

kazi kwa bidii, weledi na maarifa jambo ambalo limefanya Tanzania kuendelea kufanya vizuri kiuchumi.

Bila shaka pongezi hizi zinawahusu pia walimu ambao wamekuwa wakifanya kazi ya kufundisha wanafunzi kwa juhudi kubwa na kufanya sekta ya elimu kuendelea kupiga hatua kwa kasi.

Imani yetu ni kuwa zawadi hii iliyotolewa na Rais wetu mpendwa itakuwa chachu kwa watumishi hususan walimu kufanya kazi kwa bidii na marifa zaidi ili kuhakikisha wanafunzi wanapata kile kilichokusudiwa na hivyo kufanya Tanzania kuendelea kusonga mbele kimaendeleo.

Asante sana Rais Samia Suluhu Hassan, Kazi iendelee!!!!

KATUNI



BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti

Paulina M. Nkwama

Wajumbe

Revocatus P. Misonge
Mectildis F. Kapinga
Lameck S. Mbeya
Zachary A. Dida
Fatuma I. Muya

Mhariri Mkuu

Artemony T. Vincent

Mhariri

Adili J. Mhina

Msanifu Kurasa

Lucas G. Ogunde

Wasiliana nasi kwa Simu: +255 782 366 622 & +255 735-255238 **Barua Pepe:** secretary@tsc.go.tz
Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, **S.L.P 353, DODOMA.**



RAIS SAMIA SULUHU HASSAN ATOA NEEMA KWA WATUMISHI WA UMMA, ATANGAZA ONGEZECO LA KIMA CHA CHINI CHA MSHAHARA



Watumishi mbalimbali wakiwemo wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakiwa katika maadhimishi ya Siku ya Wafanyakazi Duniani (MEI MOSI) kitaifa yaliyofanyika mkoani Singida tarehe 1 Mei, 2025.

BUNGE LAPITISHA KWA KISHINDO BAJETI YA TAMISEMI TRILIONI 11.78 KWA MWAKA 2025/2026



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa (Mb) akijibu hoja za wabunge mbalimbali baada ya wabunge hao kujadili bajeti ya ofisi hiyo kwa mwaka 2025/2026.

Na Mwandishi wetu – Dodoma.

Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wamepitisha kwa kauli moja bajeti ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa mwaka wa fedha 2025/26 yenye takribani Shilingi trilioni 11.783 kwa ajili ya wizara na taasisi zilizo chini yake.

Kwa mujibu wa Waziri Mchengerwa Bajeti hiyo imeongezeka kutoka Shilingi trilioni 10.125 zilizotengwa mwaka 2024/25 hadi kufikia Shilingi trilioni 11.783 na kuwa na ongezeko la zaidi ya Sh trilioni 1.66.

Shilingi trilioni 3.95 zimepitishwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo kati ya fedha hizo Shilingi trilioni 2.5 ni fedha za ndani, ikijumuisha Shilingi bilioni 613.44 za mapato ya ndani ya halmashauri na Shilingi trilioni 1.45 ni fedha za nje.

Pia Shilingi trilioni 7.84 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida

yanayojumuisha mishahara Shilingi trilioni 6.3 na matumizi mengineyo Shilingi trilioni 1.53 ikijumuisha Shilingi trilioni 1.067 za mapato ya ndani ya halmashauri.

Akijibu hoja za wabunge Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Mhe Mohamed Mchengerwa amesema kuwa anatambua uwepo wa changamoto za ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara katika maeneo mbalimbali nchini. Katika kushughulikia changamoto hiyo serikali imeendelea kutenga fedha kupitia TARURA kwa ajili ya ujenzi, matengenezo na ukarabati wa Barabara ambapo bajeti imeongezeka kutoka shilingi bilioni 275.00 mwaka 2020/21 hadi shilingi bilioni 772.19 mwaka 2024/25 sawa na ongezeko la asilimia 180.8 ya fedha za ndani.

Pia Waziri Mchengerwa amesema kuwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI inatambua umuhimu wa kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia ambapo imeendelea kujenga na kukarabati miundombinu ya elimu pamoja na kuendeleza

mazingira ya maeneo hayo.

Serikali imeendelea kuwekeza katika utoaji wa Elimumsingi na Sekondari ambapo Mpango wa Elimumsingi bila Ada umeongezewa bajeti yake kutoka shilingi bilioni 249.66 mwaka 2020/21 hadi shilingi bilioni 510.96 mwaka 2025/26 kwa mwaka sawa na ongezeko la shilingi bilioni 261.30 sawa na asilimia 104.66.

Waziri Mchengerwa ametoa maelekezo kwa wakuu wa mikoa na Wilaya: kujikita kikamilifu katika kulinda amani, mshikamano wa kitaifa na ufanisi wa utendaji wa serikali katika maeneo yao.

"Hamtakiwi kuwa watazamaji wa migogoro—bali wazima moto wa chokochocho, na walinzi wa misingi ya haki, maendeleo na umoja wa kitaifa" Amesisitiza Waziri Mchengerwa.

Na kuongeza kuwa Utulivu wa nchi unaanza pale ambapo viongozi wa chini wanatimiza wajibu wao bila kusubiri maagizo kutoka juu.



Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI (Mb), Mhe. Zainab Katimba (Elimu) akijibu hoja za wabunge baada ya wabunge hao kujadili bajeti ya ofisi hiyo kwa mwaka 2025/2026 hivi karibuni.

BUNGE LAPITISHA KWA KISHINDO BAJETI YA TAMISEMI TRILIONI 11.78 KWA MWAKA 2025/2026



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa (Mb) akijibu hoja za wabunge mbalimbali baada ya wabunge hao kujadili bajeti ya ofisi hiyo kwa mwaka 2025/2026.



Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI (Mb), Mhe. Dkt. Festo Dugange akijibu hoja za wabunge baada ya wabunge hao kujadili bajeti ya ofisi hiyo kwa mwaka 2025/2026 hivi karibuni.



Baadhi ya wabunge wakijadili bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI bungeni hivi karibuni.

MWONGOZO WA MAFUNZO ELEKEZI KWA WALIMU WAPYA KAZINI USAIDIE WALIMU KUELEWA UTUMISHI WAO: PROF. MURUKE



Mwenyekiti wa Tume wa Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke akizungumza jijini Dar es salaam wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya usimamizi wa Mashauri ya Nidhamu na Rufaa kwa Makamishna wa Tume ya Utumishi wa Walimu tarehe 23 Aprili, 2025.

Na Mwandishi Wetu-Dar es salaam

Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud H. Muruke alisema kuwa Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu wanaojiririwa kwenye Utumishi wa Umma ukitumika vizuri utakuwa msaada kwa walimu wapya kazini kuelewa Sheria, Kanuni na Taratibu za utumishi wao.

Akizungumza tarehe 23 Aprili, 2025 jijini Dar es Salaam wakati wa mafunzo ya siku tatu kwa Wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Muruke alisema kuwa Mwongozo huo utasaidia kuweka usawa (uniformity) katika kutoa semina elekezi kwa walimu wapya kazini.

Alisisitiza kuwa mwongozo huo umeandaliwa ili kuondoa utofauti katika kuwaelekeza walimu wapya mara wanapoajiriwa kwa lengo la kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za utumishi wa umma.

"Mwongozo umetoa maelekezo mahsusi kwa Walimu wapya kuhusu



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Mbena Nkwama akizungumza jijini Dar es salaam wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya usimamizi wa Mashauri ya Nidhamu na Rufaa kwa Makamishna wa Tume ya Utumishi wa Walimu tarehe 23 Aprili, 2025.

Misingi ya Utumishi wa Umma na Utumishi wa Walimu, haki na wajibu wao pamoja na miiko na maadili katika utekelezaji wa majukumu yao," alisisitiza.

Katibu wa Tume ya Utumishi

wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama alisema kuwa kabla ya maandalizi ya Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu wanaojiririwa kwenye Utumishi wa Umma, kila Halmashauri ilikuwa ikitoa mafunzo elekezi kwa walimu wapya kwa utaratibu wake ambao ilikuwa inaona kuwa inafaa.

Alisema kuwa hatua hiyo ilifanya kuwepo na utofauti wa mafunzo kutoka kwa mwalimu mmoja kwenda kwa mwingine juu ya utumishi wao.

Aliongeza kuwa kupitia mwongozo huo walimu wataweza kufahamu haki, wajibu, maadili yanayoongoza Utumishi wa Umma na taaluma ya kada yao kwa ajili ya kuimarisha utendaji kazi na hivyo kuwa na Utumishi wa Umma wenye tija na utoaji wa huduma bora kwa wateja.

Mwl. Paulina alisema kuwa Mwongozo huo pia unalenga kuwapatia walimu wapya taarifa za msingi kuhusu haki na wajibu wao kama watumishi wa umma, kuwawezesha kufahamu mbinu bora za kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na kuwasisitiza umuhimu wa kujitambua kama watumishi wanaowajibika kwa jamii.

Kwa upande wake, Meneja wa Mafunzo ya Muda Mfupi kutoka Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC) Bw. Fadhil Mtinda alisema kuwa kwa muda wa siku tatu watatoa mafunzo kwa wajumbe wa Tume kuhusu usimamizi wa nidhamu kwa walimu na utaratibu wa kushughulikia mashauri ya nidhamu katika ngazi ya shule na usimamizi wa nidhamu kwa walimu na utaratibu wa kushughulikia mashauri ya nidhamu katika ngazi ya Wilaya.

Alisema kuwa mada nyingine ni utaratibu wa kushughulikia Rufaa katika utumishi wa Walimu, utaratibu na hatua za kushughulikia masuala ya nidhamu yenye jinai, utaratibu wa kushughulikia Rufaa katika Utumishi wa Walimu, Menejimenti na Utambuzi wa hisia (Emotional Intelligence) katika kusimamia uendeshaji wa Mashauri ya Nidhamu na Rufaa kwa Makamishna.

MWONGOZO WA MAFUNZO ELEKEZI KWA WALIMU WAPYA KAZINI USAIDIE WALIMU KUELEWA UTUMISHI WAO: PROF. MURUKE



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Mbena Nkwama akizungumza jijini Dar es salaam wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya usimamizi wa Mashauri ya Nidhamu na Rufaa kwa Makamishna wa Tume ya Utumishi wa Walimu tarehe 23 Aprili, 2025.

Baadhi ya Wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Walimu wakiwa katika mafunzo kuhusu Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu wanaoajiriwa kwenye Utumishi wa Umma tarehe 23 Aprili, 2025 jijini Dar es Salaam.



Meneja wa Mafunzo ya Muda Mfupi kutoka Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC), Bw. Fadhil Mtinda akitoa ufafanuzi kuhusu Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu wanaoajiriwa kwenye Utumishi wa Umma kwa Wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Walimu tarehe 23 Aprili, 2025 jijini Dar es Salaam.



16 APRILI 2025

DODOMA

“

"Wajawazito **7,440,632** walipatiwa vidonge vya kuongeza wingi wa damu. Aidha, watoto 8,944,200 wenye umri chini ya miaka mitano walipatiwa nyongeza ya matone ya Vitamini A kupitia kampeni za kitaifa zinazofanyika mara mbili kila mwaka na Kutenga **shilingi 1000** au zaidi kwa kila mtoto chini ya umri wa miaka mitano (5) kutoka mapato ya ndani ambapo jumla ya **shilingi bilioni 48.56** zilitolewa na kutumika kutoa huduma katika afua za lishe katika mikoa na halmashauri"

UWASILISHAJI WA BAJETI YA WIZARA YA OFISI YA RAIS- TAMISEMI 2025/26

MHE. MOHAMMED MCHENGERWA (MB)
WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS - TAMISEMI



16 APRILI 2025

DODOMA

“

"Ofisi ya Rais TAMISEMI imeendelea kuyaishi maneno hayo ambapo imetekeleza ilani katika huduma za ustawi wa jamii kama ifuatavyo:

Kutambua wazee 4,975,473 (wanawake 2,682,210 na wanaume 2,293,263) na kutoa huduma za matibabu bila malipo;
Kushughulikia ukatili wa kijinsia ambapo mashauri 517,286 ya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto yameshughulikiwa;
Watu wenye Ulemavu 821,763 (wanawake 410,442 na wanaume 411,321) walipatiwa huduma za msaada wa kisaikolojia na Watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi 2,592,963 (wanawake 1,450,949 na wanaume 1,142,014) walitambuliwa na kupatiwa huduma mbalimbali zikiwemo mafunzo ya ufundi stadi, kadi za bima ya afya ya jamii na vifaa vya shule."

UWASILISHAJI WA BAJETI YA WIZARA YA OFISI YA RAIS- TAMISEMI 2025/26

MHE. MOHAMMED MCHENGERWA (MB)
WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS - TAMISEMI



16 APRILI 2025

DODOMA

“

"Ofisi ya Rais TAMISEMI imetekeleza ilani katika huduma ya elimu kama ifuatavyo:
Kuboresha shule 28 za mchepuo wa elimu ya ufundi/amali kwa kuzikarabati na kutoa vifaa vya kisasa. Aidha, **kuboresha shule 274** za michepuo ya kilimo na 28 za michepuo ya biashara;
Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya elimumsingi na sekondari imeongezeka kutoka **miundombinu 582,733** hadi **754,075**. Miundombinu hiyo inajumuisha vyumba vya madarasa, shule za msingi, shule za sekondari, matundu ya vyoo kwa shule za msingi na sekondari, nyumba za walimu, maabara, mabweni na mabwalo"

UWASILISHAJI WA BAJETI YA WIZARA YA OFISI YA RAIS- TAMISEMI 2025/26

MHE. MOHAMMED MCHENGERWA (MB)
WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS - TAMISEMI



16 APRILI 2025

DODOMA

“

"katika kipindi cha miaka mitano (5) bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI pamoja na mafungu yake imekuwa ikiongezeka kutoka shilingi **trilioni 7.01 Mwaka 2020/21** hadi shilingi **trilioni 10.53 Mwaka 2024/25** sawa na ongezeko la asilimia 50.21. Ofisi ya Rais - TAMISEMI inamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuona umuhimu wa Serikali za Mitaa na kuziongezeka bajeti. Hii inaonesha namna anavyowajali wananchi kwa kupeleka maendeleo kwa vitendo katika maeneo yao."

UWASILISHAJI WA BAJETI YA WIZARA YA OFISI YA RAIS- TAMISEMI 2025/26

MHE. MOHAMMED MCHENGERWA (MB)
WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS - TAMISEMI



16 APRILI 2025

DODOMA

“

"Ofisi ya Rais TAMISEMI imetekeleza ilani katika uimarishaji wa mamlaka za serikali za mitaa kama ifuatavyo:-

Kutoa mikopo ya shilingi bilioni 158.50 kwa vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu ambapo shilingi bilioni 63.40 zimetolewa kwa vikundi 8,576 vya wanawake; shilingi bilioni 63.40 zimetolewa kwa vikundi 4,981 vya vijana; na shilingi bilioni 31.70 zimetolewa kwa vikundi 2,319 vya Watu Wenye Ulemavu;"

UWASILISHAJI WA BAJETI YA WIZARA YA OFISI YA RAIS- TAMISEMI 2025/26

MHE. MOHAMMED MCHENGERWA (MB)
WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS - TAMISEMI

MAFUNZO KWA WAJUMBE WA TSC KILOSA YAMESAIDIA KUPUNGUZA UKIUKWAJI WA MAADILI KWA WALIMU

Na Mwandishi Wetu – Kilosa.

Mafunzo kwa Wajumbe wa Kamati ya Wilaya ya Kilosa ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) yamesaidia kupunguza ukiukwaji wa maadili kutoka mashauri 25 mwaka 2022/2023 hadi 04 kwa mwaka 2024/2025.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kilosa, Bw. Daudi Mchillu wakati wa mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini cha Tume.

Aliongeza kuwa kupitia mafunzo hayo Wajumbe wameweza kufanya uchambuzi na kutoa uamuzi sahihi kulingana na aina ya kosa la kinidhamu kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu.

Aidha, Kaimu Katibu huyo Bw. Mchillu alisema kuwa Mafunzo kwa Wakuu wa Shule katika Wilaya ya Kilosa yamesaidia kuwajengea uwezo wa kuweza kubaini makosa mazito na mepesi.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kilosa, Bw. Daudi Mchillu (katikati) akiwa na maafisa wa TSC wa Wilaya hiyo, Bw. Richard William (kushoto) na Bw. Derick Ishemo Micah wakiwa katika picha ya pamoja hivi karibuni.

Bw. Mchillu alisema kuwa Uongozi wa Tume Wilaya ya Kilosa umekuwa ukifanya ziara za kutoa elimu katika Shule mbalimbali ili kuwajengea uwezo walimu kuzingatia maadili ya kazi ya ualimu.

Alisema kuwa katika zoezi hilo waliweza kufikia jumla ya kata 24 kati ya 40 ambapo walimu 1,125 walipatiwa elimu.

Bw. Mchillu aliongeza kuwa walitoa elimu kwa wadau mbalimbali wakiwemo Maafisa Elimu Wilaya, Maafisa Elimu Kata, Kamati za Shule na Bodi za Shule.

"Walimu wanajivunia kujengewa uwezo kuhusu maadili ya ualimu, miiko ya ualimu, kupata unasihi na Sheria, Kanuni na Taratibu zinazohusu Utumishi wa Walimu," alisema.

Wakati huo huo, Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kilosa imeishukuru Serikali ya Awamu ya

Sita kwa kujali maslahi ya Walimu hususan katika kuwapandisha vyeo walimu jambo ambalo limeongeza, ari ya walimu katika kufanya kazi.

Bw. Mchillu alisema kuwa katika kipindi cha kuanzia mwaka 2021 hadi mwaka 2025, jumla ya walimu 2,386 wamepandishwa vyeo miongoni mwao wa shule za Msingi ni 1,591 na Sekondari 795.

Alisema kuwa Serikali imeendelea kushughulikia madeni ya walimu ambapo kufikia mwezi Aprili 2025 jumla ya walimu 528 wakiwemo 264 wa Shule za Msingi na 264 wa Shule za Sekondari wamelipwa fedha za likizo.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) katika Wilaya ya Kilosa inahudumia jumla ya walimu 2,578 miongoni mwa hao 1,609 ni wa shule za msingi na 961 ni wa shule za sekondari.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Kilosa, Bw. Daudi Mchillu akiwa Ofisini hivi karibuni.

MAFUNZO KWA WAJUMBE WA TSC KILOSA YAMESAIDIA KUPUNGUZA UKIUKWAJI WA MAADILI KWA WALIMU



Afisa wa TSC Kilosa, Bw. Richard William akiwasilisha mada kuhusu wajibu wa Mwalimu kwa walimu wa ajira mpya hivi karibuni katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa.



Baadhi ya walimu ajira mpya wakifutulia mafunzo elekezi kuhusu ajira, haki na wajibu wao hivi karibuni katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa.



Walimu pamoja na wadau mbalimbali wakisikiliza mada ya ufafanuzi wa kanuni za maadili na utendaji kazi katika utumishi wa walimu kutoka kwa Kaimu Katibu Msaidizi Wilaya ya Kilosa (hayupo pichani) hivi karibuni.

MPANGO WA ELIMU BILA ADA UNAENDELEA KUTEKELEZWA KWA UFANISI – MHE: MCHENGERWA

Na mwandishi wetu – Dodoma.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa (Mb) ameeleza bungeni kuwa usimamizi na uendeshaji wa elimu ya msingi na sekondari unaendelea kutekelezwa kwa ufanisi

nchini.

Waziri Mchengerwa aliyasema hivi karibuni wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ambapo alifafanua kuwa Mpango wa Elimu Bila Ada unaendelea kutekelezwa kwa mafanikio makubwa, lengo kuu likiwa ni kuhakikisha kila Mtanzania

anapata haki ya msingi ya kupata elimu bora bila vikwazo vya kifedha.

Aliongeza kuwa Serikali imeendelea kuwekeza rasilimali na kuweka mifumo madhubuti ya usimamizi ili kuhakikisha mpango huu unawanufaisha wanafunzi wote nchini, sambamba na kuinua kiwango cha elimu kwa ujumla.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa (Mb).

TSC BIHARAMULO YAFANYA ZIARA KATIKA SHULE YA MSINGI MIHONGORA



Picha ya pamoja kati ya Walimu wa Shule ya Msingi Mihongora na Watumishi wa TSC Wilaya ya Biharamulo wakati wa ziara ya TSC katika shule hiyo tarehe 25 Aprili, 2025.

Na Mwandishi wetu – Biharamulo.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Biharamulo tarehe 25 Aprili, 2025 ilifanya ziara katika Shule ya Msingi Mihongora iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo kwa lengo la kutoa elimu kwa walimu wa shule hiyo juu ya masuala ya Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia Ajira, Maadili na Maendeleo katika utumishi wa walimu.



Ofisi ya Rais
TAMISEMI**HOTUBA YA BAJETI**
OFISI YA RAIS – TAMISEMI**Uratibu na Usimamizi wa
Huduma za Afya ya Msingi**

Kuongeza vituo vya kutolea huduma ya afya ya msingi kutoka 6,081 hadi 7,713 sawa na ongezeko la vituo 1,632 au asilimia 26.80. Kati ya vituo hivyo, zahanati ni 1,158, vituo vya afya 345 na hospitali za halmashauri 129; Kujenga hospitali mpya za halmashauri 129 ikiwa ni ongezeko la asilimia 31.63 ya lengo la kujenga hospitali 98;

Mhe. Mohamed Mchengerwa (Mb)Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala
za Mikoa na Serikali za Mitaa

Bungeni, Dodoma



// ortamisemi



www.tamisemi.go.tz

Ofisi ya Rais
TAMISEMI**HOTUBA YA BAJETI**
OFISI YA RAIS – TAMISEMI**Wakala ya Barabara za Vijijini
na Mijini (TARURA)** ”

Ujenzi wa barabara za changarawe ambao umeongezeka kutoka kilomita 24,493 hadi kilomita 44,372.21 sawa na ongezeko la asilimia 81.16. Urefu wa barabara za vijijini na mijini zilizojengwa kwa kiwango cha lami umeongezeka kutoka kilomita 2,025 hadi kilomita 3,467.30 sawa na ongezeko la asilimia 71.22. Aidha, kuongeza mtandao wa barabara kutoka kilomita 108,946.19 hadi kilomita 144,429.77 sawa na ongezeko la asilimia 32.57;

Mhe. Mohamed Mchengerwa (Mb)Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala
za Mikoa na Serikali za Mitaa

Bungeni, Dodoma ”



// ortamisemi



www.tamisemi.go.tz



Ofisi ya Rais
TAMISEMI

HOTUBA YA BAJETI OFISI YA RAIS – TAMISEMI



Huduma ya Mabasi Yaendayo Haraka



Ofisi ya Rais – TAMISEMI imetekeleza ilani kwa kutoa Huduma ya Mabasi Yaendayo Haraka kupitia DART kama ifuatavyo: -

- Kusambaza kadi janja 62,000 kati ya 200,000 katika awamu ya kwanza na kusimika mageti janja kwenye vituo vyote 27;
- Kusimika Mfumo wa Kielektroniki wa Ukusanyaji Nauli (Automated Fare Collection System-AFCS) ambao utafungamanishwa na mfumo wa kuongozea magari (Intelligent Transport System - ITS) ambao upo kwenye hatua ya ununuzi;

Mhe. Mohamed Mchengerwa (Mb)

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa



Bungeni, Dodoma



// ortamisemi



www.tamisemi.go.tz

Ofisi ya Rais
TAMISEMI**HOTUBA YA BAJETI**
OFISI YA RAIS – TAMISEMI**Wakala ya Barabara za Vijijini
na Mijini (TARURA)**

Kila kilomita mpya ya barabara iliyojengwa ni daraja kati ya umaskini na maendeleo; ni njia ya mtoto kufika shuleni, mama kufika hospitali, mkulima kupeleka mazao sokoni na taifa kusonga mbele. Kuongeza mtandao wa barabara kutoka kilomita 108,946 hadi zaidi ya 144,000 si takwimu tu ni mabadiliko ya kweli yanayoonekana, yanayogusika na yanayogusa maisha. Barabara hizi ni sauti ya serikali inayosema: 'Hatukuwaacha Nyuma. Hizi ni njia zinazotufikisha kwenye Tanzania ya viwanda, fursa na mshikamano wa kitaifa.

Mhe. Mohamed Mchengerwa (Mb)Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala
za Mikoa na Serikali za Mitaa

Bungeni, Dodoma



// ortamisemi



www.tamisemi.go.tz

Ofisi ya Rais
TAMISEMI**HOTUBA YA BAJETI**
OFISI YA RAIS – TAMISEMI**Usimamizi na Uendeshaji wa
Elimu Msingi na Sekondari**

Kutoa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum ambapo uandikishaji umeongezeka kutoka 28,482 hadi 78,429 sawa na asilimia 175. Aidha, madarasa 44, matundu ya vyoo 132 na mabweni 172 yamejengwa kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Mhe. Mohamed Mchengerwa (Mb)Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala
za Mikoa na Serikali za Mitaa

Bungeni, Dodoma



// ortamisemi



www.tamisemi.go.tz

Ofisi ya Rais
TAMISEMI**HOTUBA YA BAJETI**
OFISI YA RAIS – TAMISEMI**Uratibu na Usimamizi wa
Huduma za Afya ya Msingi**

Kuongeza vituo vya kutolea huduma ya afya ya msingi kutoka 6,081 hadi 7,713 sawa na ongezeko la vituo 1,632 au asilimia 26.80. Kati ya vituo hivyo, zahanati ni 1,158, vituo vya afya 345 na hospitali za halmashauri 129; Kujenga hospitali mpya za halmashauri 129 ikiwa ni ongezeko la asilimia 31.63 ya lengo la kujenga hospitali 98;

Mhe. Mohamed Mchengerwa (Mb)Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala
za Mikoa na Serikali za Mitaa

Bungeni, Dodoma



// ortamisemi



www.tamisemi.go.tz

TSC MPANDA YAWEKA NGUVU KWENYE ELIMU YA KINGA YA KUWAZUIA WALIMU KIJINGIZA MAKOSA YA KINIDHAMU

Na Mwandishi Wetu – Mpanda.

Tume ya Utumishi wa Walimu(TSC) Wilaya ya Mpanda kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea na ziara za kutoa Elimu kwa walimu katika Shule za umma kuhusu masuala ya Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia utumishi wao ili kuwajengea uwezo wa kuwazuia wasijiingize katika Mashauri ya nidhamu.

Akizungumza wakati wa mahojiano na Maafisa Habari kutoka TSC Makao Makuu Katibu Msaidizi Wilaya ya Mpanda Bw.Benson Ng'amilo amesema lengo la TSC kutoa Elimu kwa walimu wa Shule za umma kuhusu umuhimu wa kuzingatia Sheria ni kuwajengea uwezo wa kujiepusha kujiingiza katika vitendo vinavyohaisha aiba ya ualimu na kuhatarisha ajira zao.

Alisema kuwa katika ziara hiyo mada juu ya Sheria, Kanuni za maadili na utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu ilitolewa katika Shule zote ambazo wadau walitembelea.

Bw. Ng'amilo alisema kuwa katika mwaka 2023/2024,Ofisi ya Elimu Mkoa wa Katavi kwa kushirikiana na Mradi wa Shule Bora waliandaa ziara ya kutembelea Shule ambapo Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu kwa kila Wilaya alijumuishwa katika ziara hiyo ambapo kwa upande wa Wilaya ya Mpanda jumla ya kata 27 zilitembelewa.

Alisema kuwa katika elimu hiyo wanawasisitiza walimu kuhakikisha watekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria ya Utumishi wa Umma na ile Sheria inayosimamia Utumishi wa walimu ili kuepuka kujingia katika makosa ambayo yanaweza kuwasababisha wachukuliwa hatua za kinidhamu.

Bw. Ng'amilo aliongeza kuwa mbinu nyingine zinazotumika kutoa elimu ili walimu wasijiingize katika Mashauri ya Kinidhamu ni kugawa vitabu vya ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu, ambapo Shule za Msingi 114 za Wilaya ya Mpanda ziligawiwa vitabu hivyo.

Katika hatua nyingine Katibu huyo



Katibu Msaidizi Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Mpanda Bw.Benson Ng'amilo akitoa maelezo hivi karibuni kuhusu mafanikio ya Tume katika Wilaya hiyo.

Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Mpanda alisema kuwa mwaka wa fedha 2023/2024 walimu 107 wamethibitisha kazini walimu ambapo 82 ni wa Shule za Msingi na walimu 25 wa Shule za Sekondari.

Aliongeza kuwa katika kipindi hicho, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Mpanda imewapandisha vyeo jumla ya walimu 757 wakiwemo walimu 496 wa Shule za Msingi na walimu 261 wa Shule za Sekondari.

Bw. Ng'amilo alisema kuwa, Tume iliwabadilishia miundo ya utumishi walimu 38 waliojiendeleza kitaaluma, kati ya hao walimu 35 ni wa Shule za Msingi na walimu 3 ni wa shule za Sekondari.

Wakati huo huo Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu(TSC) alisema kuwa katika kipindi hiki cha Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan Ofisi ya Tume

ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Mpanda inajivunia kuajiri walimu 107 na kwa kipindi cha kuanzia Januari hadi Machi, 2025 .

"Kama ilivyo kwa TSC walimu pia wanajivunia utawala wa awamuyasita kwa kutatua kero zao zinazohusiana na upandaji vyeo, kubadili miundo ya utumishi (Recategorization), kulipwa malimbikizo ya mishahara (arreas), likizo, gharama za matibabu, uhamisho na kulipwa mafao ya kustaafu kwa wakati," alisema.

Bw. Ng'amilo alisema kuwa Wilaya ya Mpanda imeundwa na Halmashauri mbili (2) ambazo ni Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda na Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo.

Alisema Wilaya ya Mpanda ina jumla ya Shule 149, kati ya shule hizo za Msingi ni 114, shule za Sekondari ni 35.

Bw. Ng'amilo alisema Wilaya ya Mpanda ina jumla ya walimu 1,679, kati ya hao walimu wa Shule za Msingi ni 1,196 na walimu wa Shule za Sekondari ni walimu 483.



Mwenyekiti wa Tume wa Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke (kushoto) akipokea cheti cha ushiriki wa Mafunzo ya Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu wanaoajiriwa kwenye Utumishi wa Umma kutoka kwa Makamu Mwenyekiti wa TSC, Bi. Bahati Mgongolwa tarehe 23 Aprili, 2025 jijini Dar es Salaam.



Mwenyekiti wa Tume wa Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke (kulia) akimkabidhi cheti cha ushiriki wa Mafunzo ya Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu wanaoajiriwa kwenye Utumishi wa Umma Makamu Mwenyekiti wa TSC, Bi. Bahati Mgongolwa tarehe 23 Aprili, 2025 jijini Dar es Salaam.



Mwenyekiti wa Tume wa Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke (kulia) akimkabidhi cheti cha ushiriki wa Mafunzo ya Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu wanaoajiriwa kwenye Utumishi wa Umma Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Mbena Nkwama tarehe 23 Aprili, 2025 jijini Dar es Salaam.



Mwenyekiti wa Tume wa Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke (kulia) akikabidhi vyeti vya ushiriki wa Mafunzo ya Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu wanaoajiriwa kwenye Utumishi wa Umma kwa Makamishna wa TSC tarehe 23 Aprili, 2025 jijini Dar es Salaam.





Mwenyekiti wa Tume wa Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke (kulia) akikabidhi vyeti vya ushiriki wa Mafunzo ya Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu wanaoajiriwa kwenye Utumishi wa Umma kwa Makamishna wa TSC tarehe 23 Aprili, 2025 jijini Dar es Salaam.



Mwenyekiti wa Tume wa Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Mbena Nkwama (wa tatu kutoka kushoto) bara baada ya kuhitimisha Mafunzo ya Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu wanaoajiriwa kwenye Utumishi wa Umma.



TSC KILOSA YAENDESHA MAFUNZO ELEKEZI KWA WALIMU WAPYA KAZINI



Na Mwandishi Wetu – Kilosa.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kilosa hivi karibuni imefanya mafunzo elekezi kwa walimu wa ajira mpya katika Wilaya hiyo ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Walimu hao wameajiriwa na Serikali hivi karibuni na wamepangiwa vituo vya kazi katika shule mbalimbali za Halmashauri ya Wilaya hiyo.



Mafunzo elekezi kwa walimu wa ajira mpya katika Wilaya Kilosa yakiwa yanaendelea.

TSC TUNDURU YAENDESHA MAFUNZO ELEKEZI KWA WALIMU

Na Mwandishi wetu – Tunduru.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Tunduru imetoa mafunzo elekezi kwa walimu 93 wakiwemo wakuu wa Shule 31, Makamu wakuu wa shule 31 na Waandamizi Taaluma 31 kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utendaji kazi kwa walimu wa wilaya hiyo.

Mafunzo hayo yalifanyika kwa siku mbili, tarehe 28 na 29 Aprili, 2025 katika Ukumbi wa Mikutano uliopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru.

Akizungumza na watumishi hao Kaimu Mkurugenzi Halmashauri ya Tunduru aliwaasa washiriki kuzingatia yote waliyoelekezwa katika mafunzo hayo ili kupandisha kiwango cha taaluma katika Wilaya hiyo na Mkoa wa Ruvuma.

Naye Mwenyekiti wa TAHOSSA Mkoa wa Ruvuma, Mwl. Gerod Ndunguru aliwashukuru wawasilishaji wa mada, Katibu Msaidizi TSC Tunduru, Mthibiti Mkuu ubora wa Wilaya Tunduru, Katibu CWT Tunduru na Afisa Elimu Sekondari kwa kutoa mafunzo hayo na aliahidi kufuatilia utekelezaji wake shuleni.

Miongoni mwa madazilizowasilishwa katika mafunzo hayo ni: - Ajira, Maendeleo ya Walimu na Hitimisho la Kazi; Usimamizi wa Maadili ya Walimu sehemu za kazi, unasihi na hatua za kinidhamu; Utekelezaji wa Majukumu ya Kitaaluma na ukiukwaji wa wajibu wa kazi za walimu Kitaaluma; Uongozi na Usimamizi wa shule shule na kazi za kitaaluma; na Taratibu za Matumizi ya Fedha za Umma na Ubunifu wa Miradi ya Elimu ya kujitegemea shuleni.



Mafunzo Elekezi kwa Walimu wa Wilaya ya Tunduru yakiwa yanaendelea.

TSC YATWAA UBINGWA KATIKA MCHEZO WA DRAFT, MASHINDANO YA MEI MOSI



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (kulia) akipokea kombe kutoka kwa mtumishi wa TSC, Bi. Pulkeria Maimu (kushoto) wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani tarehe 1 Mei, 2025 mkoani Singida. Pichani, katikati ni Kamishna wa Tume Bi. Mariam Mnilwa.



Mtumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Bi. Pulkeria Maimu akiwa na kombe alilokabidhiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan (hayupo pichani) kwa kuwa mshindi wa kwanza kwenye mchezo wa draft katika mashindano ya Mei Mosi yaliyofanyika mkoani Singida hivi karibuni.

Bingwa wa mchezo wa draft katika mashindano ya Mei Mosi yam waka 2025 ambaye pia ni mtumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Bi. Pulkeria Maimu (aliyesika kombe) akiwa katika picha na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (kulia) na Kamishna wa Tume, Bi. Mariam Mnilwa (kushoto).

Na Mwandishi wetu – Singida.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeibuka mshindi wa kwanza kwenye mchezo wa draft katika mashindano ya Mei Mosi kwa mwaka 2025.

Mashindano hayo yalihusisha michezo mbalimbali kwa watumishi

kutoka taasisi za Serikali ambapo katika mchezo wa draft TSC iliwakilishwa na Bi. Pulkeria Maimu.

Bi. Pulkeria alikabidhiwa kombe na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan tarehe 1 Mei, 2025 katika maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi) ambayo kitaifa

yalifanyikia mkoani Singida.

Kufuatia ushindi huo, Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama alimpongeza mtumishi huyo kwa kuiwakilisha na kuitangaza vyema TSC.

Michezo mingine ambayo Tume ilishiriki katika mashindano hayo ni riadha, tufe, karata na kurusha vishale.

KATIBU WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC) MWL. PAULINA NKWAMA NA WATUMISHI WA TUME WASHIRIKI MAZAISHI YA ALIYEKUWA KATIBU WA TSC KUANZIA MWAKA 2016 – 2020



nyandhifa mbalimbali alikuwa Katibu wa Tume tangu mwaka 2016 hadi 2020.

Akitoa salamu za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama alisema Marehemu Winfrida Rutaindurwa ndiye aliyekuwa Katibu wa kwanza tangu Sheria ilipoanzishwa ya kuundwa kwa Tume hiyo.

Alisema kuwa wakati akikabidhi ofisi alimweleza kuhusu jinsi ya utendaji na changamoto mbalimbali zinazokabili Tume hiyo.

“Mama Rutaindurwa alikuwa mkarimu kwa kila mtu na wakati wote alikuwa tayari kutoa ushauri kwa viongozi wa Tume pale tulipomuomba, kwa kweli tumepoteza mtu muhimu kwa Tume...lakini tunamshukuru Mungu kwa Maisha yake hapa duniani,” alisema.

Baada ya kupitishwa kwa Sheria Namba 25 ya Mwaka 2015, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), yeye ndiye alikuwa Katibu wa kwanza.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akisaini kitabu cha maombolezo ya aliyekuzwa Katibu wa Tume hiyo, Marehemu Winfrida Rutaindurwa aliyefariki dunia na kuzikwa tarehe 25 Aprili, 2025 Mbagala Majimatitu Dar es Salaam.

Na Mwandishi Wetu - Dar es Salaam

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama na Watumishi wa Tume tarehe 25 Aprili, 2025 waliungana na mamia ya waombezaji kumuaga aliyekuwa Katibu wa Tume hiyo Mwl. Winfrida Rutaindurwa aliyefariki dunia tarehe 20 Aprili, 2025.

Mazishi hayo yalifanyika nyumbani kwa marehemu Mbagala Majimatitu jijini Dar es Salaam tarehe 25 Aprili, 2025.

Kabla ya kifo chake Bibi. Winfrida Rutaindurwa pamoja na kushika



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akiwa katika Misa ya kumwomba aliyekuwa Katibu wa Tume hiyo, Marehemu Winfrida Rutaindurwa aliyefariki dunia na kuzikwa tarehe 25 Aprili, 2025 Mbagala Majimatitu Dar es Salaam.

KATIBU WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC) MWL. PAULINA NKWAMA NA WATUMISHI WA TUME WASHIRIKI MAZAISHI YA ALIYEKUWA KATIBU WA TSC KUENZIA MWAKA 2016 – 2020



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akitoa salamu za Tume wakati wa mazishi ya aliyekuwa Katibu wa Tume hiyo, Marehemu Winifrida Rutaindurwa aliyefariki dunia na kuzikwa tarehe 25 Aprili, 2025 Mbagala Majimatitu Dar es Salaam.



Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Rasilimaliwaatu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Bw. Zachary Dida akisaini kitabu cha maombolezo ya aliyekuwa Katibu wa Tume hiyo, Marehemu Winifrida Rutaindurwa aliyefariki dunia na kuzikwa tarehe 25 Aprili, 2025 Mbagala Majimatitu Dar es Salaam.



MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu